**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**
**WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**ILIYOWASILISHWA NA**
**MHESHIMIWA ANNA ATHANAS PAUL (MBM)**
**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

**MEI, 2026**



Mhe. Anna Athanas Paul

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia,Wazee na Watoto



Mhe. Zawadi Amour Nassor

Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia,Wazee na Watoto



Ndg. Abeida Rashid Abdallah
Katibu Mkuu

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia,Wazee na Watoto



Ndg. Khatib Mwadini Khatib
Naibu KatibuMkuuWizara ya Maendeleo
ya Jamii, Jinsia,Wazee na Watoto



Ndg. Hafidh Ali Mohamed
Afisa Mdhamini Wizara ya Maendeleo
ya Jamii, Jinsia,Wazee na Watoto



Ndg. Daima Mohamed Mkalimoto
Mkurugenzi Mipango, Sera na Utafiti
Wizara ya Maendeleo
ya Jamii, Jinsia,Wazee na Watoto



Ndg. Hassan Ibrahim Suleiman
Mkurugenzi Ustawi wa Jamii na Wazee
Wizara ya Maendeleo
ya Jamii, Jinsia,Wazee na Watoto



Ndg. Juma Ali Simai
Mkurugenzi Utumishi na Uendeshaji
Wizara ya Maendeleo
ya Jamii, Jinsia,Wazee na Watoto



Ndg. Siti Abbas Ali
Mkurugenzi Maendeleo ya Jamii Jinsia
na WatotoWizara ya Maendeleo
ya Jamii, Jinsia,Wazee na Watoto

## YALIYOMO

**A. UTANGULIZI** .......... 1
**B. VIPAUMBELE VYA WIZARA** .......... 2
**C. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MSINGI YA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2025 – MACHI 2026** .......... 4
*Ukusanyaji wa Mapato* .......... 4
*Mafanikio na Changamoto* .......... 4
*Mapato na Matumizi* .......... 5
Utekelezaji wa Miradi inayosimamiwa na Wizara .......... 6
Utekelezaji wa Bajeti kwa Programu za Fungu la Wizara .......... 8
*Programu ya Hifadhi ya Jamii* .......... 8
*Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara* .......... 11
*Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji* .......... 11
*Programu ndogo ya Uratibu Mipango, Sera na Utafiti* .......... 13
*Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji Ofisi Kuu Pemba* .... 15
*Programu ya Maendeleo ya Jamii na Jinsia (PH0403)* .......... 17

**D. MWELEKEO WA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2026/2027** .......... 19
*Programu ya Hifadhi ya Jamii (PH0401)* .......... 23
*Programu ya Utawala na Uendeshaji* .......... 23
Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji (SH040201) .......... 23
Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti .......... 24
Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji Ofisi Kuu Pemba(SH040203) .......... 25
*Programu ya Maendeleo ya Jamii na Jinsia* .......... 25

**E. SHUKURANI** .......... 26
**F. HITIMISHO** .......... 28
Kiambatanisho Nam. 1: Muhtasari wa Upatikanaji wa Fedhakwa Kipindi cha Julai, 2025 - Machi 2026 .......... 29

Kiambatanisho Nam. 2: Mwelekeo wa Bajeti kwa mwaka 2026/2027 ............................................30

Kiambatanisho Nam. 3: Taarifa ya Wazee walio katika Mpango wa Pencheni Jamii ....................31
Kiambatanisho Nam. 4: Malalamiko ya Matunzo na Mvutano wa Malezi ................................32
Kiambatanisho Nam. 5: Wahanga waliopo Nyumba Salama ........33
Kiambatanisho Nam. 6: Vituo Vya Kulelea Watoto Yatima ..........34
Kiambatanisho Nam. 7: Orodha ya walezi wa malezi na watoto waliopo katika malezi .................35
Kiambatanisho Nam. 8a:Idadi ya Watumishi wa Wizara...............36
Kiambatanisho Nam. 8b:Watumishi waliopo kwenye mafunzo ya muda mrefu .......................36
Kiambatanisho Nam. 8c: Watumishi waliopatiwa mafunzo ya muda mfupi .....................................37

## Vifupishio vya Maneno

| | |
|---|---|
| BAKIZA | Baraza la Kiswahili Zanzibar |
| CCM | Chama Cha Mapinduzi |
| CDC | Shirika la Afya ya Jamii |
| CRDB | Benki ya Maendeleo Vijijini Tanzania |
| CRF | Shirika la Mtandao wa Haki za Watoto Zanzibar |
| C-SEMA | Huduma ya Simu ya Mtoto |
| DPP | Mkurugenzi wa Mashtaka |
| EU | Umoja wa Nchi za Ulaya |
| GEF | Jukwaa la Kizazi chenye Usawa |
| IOM | Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Wahamiaji |
| IPA | Chuo cha Utawala wa Umma |
| ITV | Independent Television |
| JKU | Jeshi la Kujenga Uchumi |
| JUWAZA | Jumuiya ya Wastaafu na Wazee Zanzibar |
| JUYAWAZA | Jumuiya ya Wazee Zanzibar |
| KIU | Kampala International University |
| LSF | Huduma ya Msaada wa Kisheria |
| NBS | Ofisi ya Taifa ya Takwimu Tanzania |
| NMB | Benki ya Taifa ya Biashara Ndogo ndogo |
| NPA-VAWC | Mpango wa Taifa wa Kupinga Ukatili na Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto |
| PBB | Mfumo wa Bajeti unaozingatia Programu |
| PDB | Taasisi ya Ofisi ya Ufuatiliaji ya Serikali Zanzibar |
| PBZ | Benki ya Watu wa Zanzibar |
| PhD | Shahada ya Uzamivu |
| SMT | Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| SMZ | Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar |
| SUZA | Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar |
| TAMWA | Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania |
| TBC | Shirika la Habari Tanzania |
| THESODE | Theatre for Social Development |

| | |
|---|---|
| THPS | Tanzania Health Promotion Support |
| TIRA | Mamlaka ya Bima Tanzania |
| TRA | Mamlaka ya Mapato Tanzania |
| UAE | Umoja wa Falme za Kiarabu |
| UNFPA | Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Idadi ya Watu |
| UNICEF | Shirika la Umoja wa Mataifa Watoto |
| UNWOMEN | Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia masuala ya Wanawake |
| USAID | Shirika la Misaada la Marekani |
| UV CCM | Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi |
| UWT | Umoja wa Wanawake Tanzania |
| WHO | Shirika la Afya Duniani |
| ZACA | Jumuiya ya Misaada ya Watoto |
| ZAECA | Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi |
| ZAFELA | Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar |
| ZAMWASO | Jumuiya ya Misaada ya Wanawake wa Kiislamu |
| ZAPHA+ | Jumuiya ya Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI |
| ZASO | Jumuiya ya Kusaidia Watoto Yatima na Wanaishi na Virusi vya UKIMWI |
| ZASWA | Jumuiya ya Maafisa ustawi wa jamii Zanzibar |
| ZBC | Shirika la Utangazaji Zanzibar |
| ZC TV | Zanzibar Cable Television |
| ZPC | Shirika la Bandari Zanzibar |
| ZSSF | Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar |
| ZSTC | Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar |
| ZURA | Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar |
| ZU | Chuo Kikuu cha Zanzibar |

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha hotuba ya bajeti ya mapato na matumizi kwa mwaka 2025/2026 na Mwelekeo wa Bajeti ya Mwaka 2026/2027 kwa ajili ya kuijadili na hatimae kuidhinisha bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

2. **Mheshimiwa Spika,** nitumie fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kuendelea kutekeleza majukumu yetu ya kuwahudumia wananchi. Aidha, nampongeza kwa dhati Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, **Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi** kwa kuchaguliwa kwa mara ya pili kwa ushindi wa kishindo katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika tarehe 29 Oktoba, 2025. Ushindi huu unaonesha wazi imani kubwa waliyonayo wananchi wa Zanzibar katika jitihada zake za kuleta maendeleo makubwa ndani ya nchi yetu. Vile vile, ninamshukuru kwa kuniteua kuwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

3. **Mheshimiwa Spika,** nampongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa **Dkt. Samia Suluhu Hassan** kwa kuchaguliwa kwa kishindo katika Uchaguzi Mkuu wa tarehe 29 Oktoba, 2025. Aidha, nampongeza Rais kwa juhudi zake anazozichukua katika kuliongoza Taifa letu na kuimarisha usawa wa kijinsia na maendeleo kwa ujumla.

4. **Mheshimiwa Spika,** natoa pongezi kwa Makamu wa Pili wa Rais **Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla** kwa kumsaidia na kumshauri vyema Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika utekelezaji wa

majukumu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kutuletea maendeleo makubwa katika nchi yetu.

5. **Mheshimiwa Spika,** kwa moyo wa dhati kabisa nampongeza mama yetu mpendwa, mke wa Rais wa Zanzibar, Msarifu na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Zanzibar Maisha Bora, **Mama Mariam Mwinyi**, kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kuimarisha ustawi wa wanawake, watoto, wazee na jamii kwa ujumla.

6. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inatambua na kuthamini mchango mkubwa wa Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi inayoongozwa na **Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Hussein Ibrahim Makungu** na **Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Dkt. Nassra Nassor Omar** pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati kwa namna wanavyotushauri katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara yetu. Aidha, naishukuru Kamati kwa kuyapitia mapendekezo ya bajeti ya mwaka wa fedha 2026/2027 na kutupatia maelekezo yaliyotuwezesha kukamilisha maandalizi ya hotuba hii ambayo naiwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu.

## B. VIPAUMBELE VYA WIZARA

7. **Mheshimiwa Spika,** vipaumbele vya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka wa fedha 2025/2026 vilikuwa kama ifuatavyo: -

   i. Kukuza utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Kitaifa wa Kupambana na Ukatili na Udhalilishaji dhidi ya Wanawake na Watoto (NPA VAWC II 2025 - 2030); Mpango wa Pili wa Utekelezaji wa Sera ya Hifadhi ya Jamii; na Mpango wa Utekelezaji wa Ahadi za Nchi za Kizazi Chenye Usawa (GEF);

ii. Kutayarisha na kutekeleza Mpango wa Utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Jamii, kukamilisha mapitio ya Sera ya Jinsia na kukamilisha Sheria mpya ya Watoto;

iii. Kuimarisha Huduma za malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto katika ngazi za familia, jamii na taasisi;

iv. Kutekeleza Mapendekezo ya Utafiti wa Ukatili na Udhalilishaji dhidi ya Watoto na Vijana (VACS 2024) na tafiti nyingine zinazogusa makundi yanayosimamiwa na Wizara;

v. Kuimarisha Hifadhi ya Jamii, Wazee, Watoto na Familia zinazoishi katika mazingira magumu zaidi;

vi. Kuratibu utoaji wa huduma za msingi kwa watu wenye mahitaji maalum ikiwemo huduma za msaada wa kisaikolojia kwa manusura wa majanga mbalimbali na makundi mengine yenye uhitaji katika jamii;

vii. Kuimarisha mifumo ya malezi, ulinzi na maendeleo ya watoto na familia.

viii. Kuimarisha uratibu na usimamizi wa Kada za Ustawi na Maendeleo ya Jamii likiwemo suala la kutayarisha Sheria ya Ustawi wa Jamii;

ix. Kuratibu Mipango na bajeti inayozingatia Usawa wa Kijinsia katika Wizara, Taasisi, Mikoa na Wilaya; na

x. Kuimarisha nguvu kazi na mazingira ya kazi ikiwemo upatikanaji wa vitendea kazi, matengenezo ya majengo na kumbukumbu muhimu za kiutumishi.

## C. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MSINGI YA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2025 – MACHI 2026

### *Ukusanyaji wa Mapato*

8. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ilikadiriwa kukusanya kiasi cha shilingi 15,000,000.00 kupitia ukodishaji wa Ukumbi wa Mikutano uliopo Sebleni, ambapo fedha zilizokusanywa katika kipindi hicho ni shilingi 9,200,000.00 sawa na asilimia 61.

### *Mafanikio na Changamoto*

9. **Mheshimiwa Spika,** mafanikio na changamoto katika utekelezaji wa mpango na bajeti ya Wizara ni kama ifuatavyo: -

**Mafanikio**

i. Kuendelea kuratibu Mpango wa Pencheni Jamii ambapo mwaka 2020 kulikuwa na wazee 30,127 na hadi Machi 2026 wamefikia wazee 33,881 sawa na ongezeko la wazee 3,754; na kutolewa kwa Vitambulisho 31,221 vya huduma za kijamii kwa wazee;

ii. Kuwawezesha Wanawake 144 kujiajiri na kuanzisha shughuli ndogo ndogo za kiuchumi;

iii. Kuimarika kwa ushirikiano wa Kitaifa, kikanda na kimataifa katika shughuli zinazohusiana na Wizara; na

iv. Kuongezeka kwa mwitiko wa malezi na huduma kwa wazazi na walezi; na kuandaa Programu ya Miaka Mitano ya Malezi na Makuzi ya Awali ya Mtoto (ECD) kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais ya Kusimamia Utekelezaji Serikalini (PDB).

**10. Mheshimiwa Spika,** Wizara imekabiliana na changamoto zifuatazo:-

**Changamoto**

i. Kuwepo kwa familia zenye mazingira magumu zaidi ambazo zinahitaji usaidizi. Wizara inafanya jitihada za kuzifikia familia hizo na kuzipatia msaada.

ii. Uwepo wa uhitaji mkubwa wa mikopo kwa wajasiriamali wanawake. Wizara inaendelea na juhudi za ufuatiliaji wa majukwaa na vikundi vya wanawake wajasiriamali kupitia Mradi wa PAMOJA na *Programu ya Dkt. Mwinyi* Boosting Fund ambao unakusudia kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa walengwa.

iii. Wizara kukosa jengo la Ofisi ambalo linaziunganisha Idara zote sehemu moja. Hadi sasa Wizara inakodi Ofisi katika jengo la ZSTC Kinazini.

## *Mapato na Matumizi*

**11. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ilikadiriwa kutumia shilingi 17,072,042,138.00 ambapo hadi kufikia Machi 2026, shilingi 13,776,091,416.00 sawa na asilimia 81 ya makadirio ya mwaka zimepatikana. Fedha za matumizi ya kawaida zilizopangwa ni shilingi 10,581,521,000.00 zinazohusisha mishahara shilingi 4,196,100,000.00 na shilingi 6,385,421,000.00 za matumizi mengineyo. Kati ya fedha zilizopatikana shilingi 3,014,216,007.00 zilitumika kwa ajili ya mishahara ambayo ni sawa na asilimia 75 ya makadirio ya mishahara na shilingi 2,676,544,901.00 sawa na asilimia 45 ya makadirio ya matumizi mengineyo. Fedha za maendeleo

zilizopangwa ni shilingi 6,490,521,000 zinazohusisha SMZ shilingi 1,500,000,000 na shilingi 4,990,521,000 za Washirika wa Maendeleo. Fedha za maendeleo zilizopatikana ni shilingi 7,942,760,485 sawa na asilimia 104 ya makadirio ya mwaka, ambapo Fedha za SMZ zilikuwa shilingi 1,204,328,957.00 sawa na asilimia 80 ya makadirio na za Washirika wa Maendeleo zilikuwa shilingi 6,738,431,528.00 sawa na asilimia 135 ya makadirio. **Kiambatanisho nambari 1 kinahusika.**

**Utekelezaji wa Miradi inayosimamiwa na Wizara**

**12.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara inatekeleza miradi mitatu ambayo ni *Mradi wa Hifadhi ya Wazee unaohusu kufanyia ukarabati majengo ya Wazee ya Sebleni Unguja na Limbani Pemba; na Mradi wa Maliza Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji wa Wanawake na Wasichana* (TOKOMEZA) unaotekelezwa kwa mashirikiano na UN-WOMEN na Mradi wa Kukuza Usawa wa Kijinsia Tanzania (PAMOJA) unaofadhiliwa na Benki ya Dunia.

**13.** **Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Hifadhi ya Wazee ulipangiwa kiasi cha shilingi 1,500,000,000.00 na hadi kufikia Machi 2026 mradi uliingiziwa shilingi 1,204,328,957.00 ambayo ni sawa na asilimia 80. Kupitia mradi huu, Wizara imefanya ukarabati mkubwa wa majengo ya makaazi ya Wazee Sebleni na Limbani.

**14.** **Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Maliza Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji wa Wanawake na Wasichana (TOKOMEZA) ulipangiwa kiasi cha shilingi 555,000,000.00 na hadi kufikia Machi 2026, mradi uliingiziwa shilingi 113,063,489.00 ambayo ni sawa na asilimia 20. Kupitia mradi huu, Wizara imeendelea kutekeleza Mpangokazi wa Pili wa Kitaifa wa Kupambana na Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto (2025 - 2030).

15. **Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Kukuza Usawa wa Kijinsia Tanzania PAMOJA ni mradi wa miaka mitano ambao umeanza utekelezaji wake kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Mradi ulipangiwa jumla ya shilingi 4,354,200,000.00 ambapo hadi kufikia Machi, 2026, shilingi 6,512,304,550.00 zimeingizwa na shilingi 685,858,600.00 zimetumika ikiwa sawa na asilimia 10 ya fedha zilizoingizwa. Utekelezaji huu mdogo umechangiwa na uhitaji wa kukamilisha hatua za awali za matayarisho ya utekelezaji mradi.

16. **Mheshimiwa Spika,** Hatua za awali zilizochukuliwa ni pamoja na:-

(i) Kuandaa muongozo wa utoaji wa mafunzo na mikopo kwa vikundi vya uzalishaji na kufanya mikutano ya Jamii ya kuutambulisha mradi, ambapo jumla ya Shehia 89 zilifikiwa na wananchi 7,149 (wanawake 6,336 na wanaume 813) walihudhuria katika mikutano hiyo.

(ii) Kutayarisha Nyaraka na hadidu rejea za kutafuta wataalamu elekezi wanaohitajika kutoa huduma.

(iii) Kufanya utambuzi wa watoa huduma za kupinga Ukatili wa Kijinsia (GBV) katika Wilaya nane za Unguja na Pemba, kwa lengo la kutambua uwezo wao wa kitaaluma na rasilimali.

(iv) Kuanza taratibu za kumpata Mshauri Elekezi na Mkandarasi kwa ajili ya usanifu na usimamizi wa ujenzi.

(v) Kusimamia uratibu na uendeshaji wa mradi.

17. **Mheshimiwa Spika,** Wizara pia inatekeleza Programu ya Kupinga Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa

Wanawake na Watoto ambayo ilitengewa shilingi 81,321,000.00 na hadi kufikia Machi, 2026 programu iliingiziwa fedha zote zilizotengwa. Wizara ilitayarisha Mpango Mkakati wa utekelezaji wa NPA - VAWC II kwa Mkoa wa Kusini Pemba na Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja na kufanya mikutano mbalimbali ya uratibu.

**Utekelezaji wa Bajeti kwa Programu za Fungu la Wizara**

**18.** **Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo sasa naomba uniruhusu kutoa taarifa ya utekelezaji wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

**Programu ya Hifadhi ya Jamii (PH0401)**

**19.** **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inahusika na kuimarisha mifumo ya hifadhi ya jamii na huduma kwa wazee, watoto na watu wanaoishi katika mazingira magumu zaidi. Shughuli zilizotekelezwa zimezingatia Sheria ya Watoto Nambari 6 ya mwaka 2011, Sheria ya Wazee Nambari 2 ya mwaka 2020, Sera ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2014 na mikakati ya Kitaifa na Kimataifa. Programu hii ilitengewa shilingi 3,643,223,000.00 na hadi kufikia Machi, 2026 shilingi 2,160,425,334.00 zilipatikana ikiwa ni sawa na asilimia 59 ya makadirio.

**20.** **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ilipanga kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuendelea kutoa huduma za kiustawi kwa Wazee ikiwemo kuwapatia vitambulisho vya huduma za kijamii na kuimarisha mabaraza ya wazee;

ii. Kuendelea na awamu ya pili ya matengenezo katika

makaazi ya wazee Sebleni na kujenga makaazi ya wazee ya Welezo;

iii. Kutoa huduma za hifadhi na ustawi wa jamii kwa watu wenye mazingira magumu zaidi; na

iv. Kuimarisha huduma za malezi na msaada wa Kisaikolojia pamoja na kujenga uwezo wa watoa huduma.

**21.** **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2026, Wazee 67 wameendelea kutunzwa katika makaazi ya wazee ambapo Welezo wazee 38 (wanawake 25 na wanaume 13), Sebleni wazee 21 (wanawake 10 na wanaume 11) na Limbani wazee wanane (wanawake 3 na wanaume 5). Aidha, uratibu wa mpango wa Pencheni Jamii kwa wazee umefanyika na hadi kufikia Machi, 2026 jumla ya wazee 33,881 (Unguja 19,921 na Pemba 13,960) wamesajiliwa, idadi inayojumuisha wazee wapya 2,478. Katika kipindi hiki wazee 1,035 (Unguja 634 na Pemba 401) wamefariki na kuondolewa katika orodha ya wanufaika wa mpango huu. **Kiambatanisho nambari 3 kinahusika**.

**22.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara ilipokea na kufanyia kazi malalamiko 657 (Unguja 406 na Pemba 251) yanayohusu ukiukwaji wa haki za watoto. Kati ya hayo malalamiko 390 (Unguja 238 na Pemba 152) ni ya kukosa huduma za matunzo ya watoto na 267 (Unguja 168 na Pemba 99) yalihusu mvutano wa malezi ambapo watoto 881 (wanawake 408 na wanaume 473) waliathirika na malalamiko hayo. Vile vile, Wizara inaendelea kutoa huduma kwa wahanga wa vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Wahanga 49 (wanawake 38 na wanaume 11) walipokelewa Nyumba Salama kwa ajili ya hifadhi ya muda kutokana na matukio ya udhalilishaji. **Viambatanisho nambari 4 na 5 vinahusika.**

23. **Mheshimiwa Spika,** watoto 14 (wanawake 4 na wanaume 10) wenye umri wa kuanzia miaka 12 hadi 17 walipokelewa kupitia Mpango wa Marekebisho ya Tabia kwa watoto wanaokinzana na sheria na hadi kufikia Machi, 2026 kituo kimebakiwa na watoto watatu (wa kike ni mmoja na wawili wa kiume). Watoto wengine 11 wamehitimu mafunzo yao ya miezi sita. Watoto hao hupatiwa taaluma ya mambo mbalimbali ikiwemo stadi za maisha, ushauri nasaha, ufundi, ushoni, uchoraji, mafunzo ya kompyuta, sanaa ya maigizo, ujasiriamali na michezo.

24. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kusimamia Kituo cha Kulelea Watoto Mazizini chenye watoto 30 (wakike 09 na wakiume 21) na watoto saba walitolewa na kuunganishwa na familia zao. Aidha, Wizara imefuatilia uendeshaji wa vituo vya kulelea watoto 18 (Unguja 16 na Pemba 2) kwa lengo la kufuatilia huduma zinazotolewa katika vituo hivyo pamoja na kutoa ushauri na maelekezo kwa wasimamizi wa malezi ya watoto. **Kiambatanisho nambari 6 kinahusika.**

25. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inaendelea kusimamia Mpango wa Malezi ya Walezi kupitia kanuni ya walezi ya mwaka 2017, ambapo watoto 75 (wanawake 38 na wanaume 37) wamepatiwa huduma ya malezi. Aidha, walezi wa malezi 206 (Unguja 106 na Pemba 100) wamesajiliwa kupitia mpango huo. **Kiambatanisho nambari 7 kinahusika.**

26. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuratibu na kupokea maombi ya uanzishwaji wa vituo vya Malezi ya Kutwa (Day Care Centres) kwa watoto. Katika kipindi hiki Wizara imefuatilia vituo 26 vinavyotoa huduma hiyo na inaendelea kuvikagua na kuvisajili vituo 30 vilivyoleta maombi kwa mujibu wa Sheria na taratibu za Serikali pamoja na kutoa ushauri unaofaa ili

kuhakikisha watoto wanaendelea kulelewa na kukuzwa vizuri kiakili, kimwili, kimaadili na kitaaluma.

27. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutoa huduma za Ustawi wa Jamii kwa kutoa fedha taslimu kwa familia 357 (Unguja 204 na Pemba 153) zenye mazingira magumu zaidi, akinamama 18 waliojifungua watoto pacha watatu (Unguja 12 na Pemba 6) na wananchi 43 (wanawake 25 na wanaume 18) wanaoishi kijiji cha Makundeni. Vile vile, Wizara inaendelea kutoa huduma za mazishi ya maiti ambao hawana ndugu wala jamaa. Jumla ya maiti 10 wamezikwa na Serikali.

**Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara (PH0102)**

28. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina programu ndogo tatu ambazo ni Utawala na Uendeshaji, Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti; na Utawala na Uendeshaji Ofisi Kuu Pemba. Programu hii ilipangiwa shilingi 7,691,815,332.00 na hadi kufikia Machi 2026, fedha zilizopatikana ni shilingi 4,094,716,395.00 sawa na asilimia 53 ya makadirio. Utekelezaji kupitia Programu ndogo hizo ni kama ifuatavyo:-

***Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji (SH040201)***

29. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ilipanga kutumia shilingi 5,553,920,000.00 zikiwemo shilingi 3,590,405,000.00 za mishahara na shilingi 1,963,515,000.00 za matumizi mengineyo. Hadi kufikia mwezi Machi, 2026 jumla ya shilingi 3,212,667,926.00 sawa na asilimia 58 zilipatikana zinazojumuisha shilingi 2,692,105,756.00, sawa na asilimia 75 za mishahara na shilingi 520,562,170.00 sawa na asilimia 27 za matumizi mengineyo. Programu ndogo hii ya Utawala na Uendeshaji ilipanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kuendelea kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara na kuwapatia haki na stahiki zao;

ii. Kutekeleza shughuli za kiutawala na uendeshaji wa Ofisi ikiwa ni pamoja na kuipatia Wizara vitendea kazi; na

iii. Kuendelea kuimarisha kumbukumbu na nyenzo nyingine za kiutumishi ili kuweka usimamizi imara wa rasilimali watu katika Wizara.

**30.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara ina jumla ya watumishi 316 (Unguja 271; Wanawake 171 na wanaume 100 na Pemba 45; Wanawake 25 na Wanaume 20). Aidha, watumishi saba walipatiwa mafunzo ya muda mrefu na watumishi 11 mafunzo ya muda mfupi. Vile vile, watumishi 85 walipatiwa mafunzo ya ndani yaliyohusu Maadili ya Watumishi wa Umma. **Viambatanisho nambari 8 a, b & c vinahusika.**

**31.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara imewapatia stahiki za kufanya kazi muda wa ziada watumishi 33 na watumishi 101 wamepatiwa likizo la kawaida na stahiki zao. Aidha, watumishi 160 walipatiwa nyongeza za mishahara baada ya kukamilika kwa taratibu za upimaji utendaji kazi wao (Performance Appraisal).

**32.** **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha uwajibikaji na utendaji wa Wizara unaimarika vitendea kazi na vifaa mbalimbali vya Ofisi vikiwemo kompyuta, printa, mashine ya fotokopi, vifaa vya mahudhurio ya watumishi (biometric), kamera za ulinzi na usalama (CCTV) vimenunuliwa. Vile vile, vikao vya Kamati ya Uongozi, Kamati Tendaji na Kamati ya Ukaguzi vilifanyika. Aidha, vikao vya Bodi ya Zabuni vilifanyika kupitia zabuni mbalimbali zilizowasilishwa. Katika kuhakikisha kuwa misingi, sheria, kanuni na taratibu za kiutumishi zinafuatwa, Wizara

imefanya ukaguzi wa ndani kwa lengo la kuimarisha udhibiti wa rasilimali za umma.

33. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imefanya mikutano 12 ya waandishi wa habari, kutayarisha vipindi vitano vya Redio na tisa vya Televisheni, na kutangaza matukio 92 na taarifa 49 za magazeti kwa lengo la kuhabarisha jamii juu ya utendaji wa Wizara.

34. **Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza maelekezo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Wizara imeendelea kuimarisha utendaji kazi kwa kutumia Mifumo mbalimbali ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) inayosimamiwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao Zanzibar na Ofisi Kuu ya Utumishi wa Umma ikiwemo Mfumo wa Ununuzi Mtandao, Ofisi Mtandao, Mfumo wa Malipo ya Mishahara na stahiki za Watumishi na Mfumo wa Vibali Mtandao.

35. **Mheshimiwa Spika,** Katika dhana ya kujenga mashirikiano na mahusiano mema, Wizara ilipata fursa ya kushiriki na kuhudhuria makongamano na mikutano mbalimbali ndani na nje ya nchi ikiwemo Mkutano wa Uzinduzi wa Mpango kazi wa Kitaifa wa kushughulikia Agenda ya Wanawake, Amani na Usalama; na Mkutano wa 70 wa Tume ya Hadhi ya Wanawake (CSW70) uliofanyika Jijini New York nchini Marekani.

***Programu ndogo ya Uratibu Mipango, Sera na Utafiti (SH040202)***

36. **Mheshimiwa Spika** Programu hii inashughulikia kuratibu uandaaji, utekelezaji na usimamizi wa Sera, Miongozo, Mipango ya sekta pamoja na kufanya mapitio ya sheria, kanuni na sera zinazohitaji kufanyiwa marekebisho. Programu hii ilitengewa shilingi 432,100,000.00 za matumizi mengineyo na fedha

iliyopatikana ni shilingi 37,777,334.00 ikiwa ni sawa na asilimia 9. Shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni hizi zifuatazo: -

i. Kuratibu utayarishaji wa Mpango, Bajeti, na Ripoti za Wizara;

ii. Kuandaa na kuchambua sera zinazosimamiwa na Wizara na Sera nyingine za Kisekta ili kuhakikisha dhana ya maendeleo ya jamii na mipango na bajeti inayozingatia jinsia zinaendelea kukondoishwa; na

iii. Kuendelea kuratibu ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa wizara na kutekeleza mikakati ya kufanyia kazi tafiti za kijamii.

37. **Mheshimiwa Spika,** Wizara iliratibu mpango, bajeti na ripoti zilizowasilishwa katika ngazi mbalimbali za uratibu – Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, na Utekelezaji wa ILANI. Matayarisho ya Bajeti ya Wizara yamekamilika na kazi ya uwekaji wa taarifa za Wizara katika mfumo wa BAMAS imefanyika. Aidha, hatua za kutayarisha Mpango Mkakati mpya wa Wizara zinaendelea baada ya mpango uliopo kufikia ukomo wake mwaka 2026.

38. **Mheshimiwa Spika,** kazi za uratibu wa shughuli za Wizara zimeendelea ambapo kwa kipindi hiki, Programu ya Jinsia na Maendeleo imeanza kutayarishwa kwa ushirikiano na Taasisi ya BUFDIR ya Norway. Hatua za awali za ushirikiano huo zimelenga kujenga uwezo wa kuratibu maendeleo ya usawa wa kijinsia Zanzibar kwa Watendaji wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Hatua inayofuata ni kuwajengea uwezo Watendaji wa Wizara za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ili kulifanya suala la kuimarisha usawa wa kijinsia liweze

kukondoishwa, kumilikiwa na sekta zote na hatimaye kuleta mabadiliko yanayotarajiwa ya usawa wa kijinsia na maendeleo. Maandalizi ya Programu hiyo yameanza kwa kuandaa waraka wa makubaliano, kufanya mafunzo kwa watendaji wa Wizara na kuandaa mpango wa utekelezaji.

39. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea na uratibu wa uandaji wa Sera ya Mtoto na Sera ya Maendeleo ya Jamii. Sera ya Mtoto ipo katika hatua ya kukamilisha marekebisho yaliyotolewa na Kamati Tendaji na baadae kuwasilishwa Kamati ya Uongozi. Aidha, Sera ya Maendeleo ya Jamii ipo katika hatua ya kuwasilishwa katika Kamati ya Makatibu Wakuu. Ukamilishaji wa Sheria ya Mtoto umefikia hatua za kupelekwa Baraza la Mapinduzi.

40. **Mheshimiwa Spika,** Mradi wa PAMOJA ulizinduliwa tarehe 4 Machi 2026 ukihusisha wadau mbalimbali. Utekelezaji wa mradi huu unaendelea kuratibiwa kupitia Kamati za Kitaalamu na Kamati za Usimamizi kwa upande wa Jamhuri ya Muungano na Zanzibar. Aidha, ziara za ufuatiliaji zilifanyika kutathmini maendeleo na changamoto za utekelezaji.

41. **Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango ilifanya tathmini ya utekelezaji wa Wizara nane zilizotayarisha bajeti zenye kuzingatia jinsia na usawa (GRB) kwa lengo la kuimarisha mpango huo.

***Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji Ofisi Kuu Pemba (SH040203)***

42. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo hii inahusika na uratibu wa masuala yote yanayohusu majukumu ya Sekta ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa upande wa Pemba na

ilitengewa shilingi 1,705,795,000.00 (shilingi 605,695,332.00 za mshahara na shilingi 1,100,100,000.00 za matumizi mengineyo). Fedha zilizopatikana ni shilingi 844,271,135.00 (shilingi 464,680,275.00 za mshahara na shilingi 379,590,860.00 za matumizi mengineyo) ikiwa ni sawa na asilimia 49 ya fedha iliyotengwa. Shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni:-

i. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za kawaida za Wizara Pemba;

ii. Kuendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa sera, sheria, miongozo na kanuni za Wizara; na

iii. Kuwajengea uwezo watumishi, kuweka mazingira mazuri ya kazi pamoja na kuhakikisha haki na stahiki zao.

**43.** **Mheshimiwa Spika,** Ofisi Kuu Pemba ina watumishi 45 (wanawake 25 na wanaume 20) na katika kipindi hiki watumishi 13 (wanawake 7 na wanaume 6) wamepatiwa likizo na stahiki zao. Aidha, wizara imewapatia mafunzo ya muda mfupi watumishi 13 na wawili wapo katika mafunzo ya muda mrefu. Watumishi wanane (wanawake 3 na wanaume 5) wamepimwa na kupandishwa madaraja. Vile vile, Wizara imelipa gharama za umeme kwa jengo la Wizara pamoja na gharama za kukodi nyumba mbili kwa ajili ya makaazi ya muda ya wazee kwa kipindi cha ukarabati wa Nyumba ya Wazee Limbani.

**44.** **Mheshimiwa Spika,** Ofisi Kuu Pemba imeandaa Bajeti kwa mwaka 2026/2027 na kuingiza vifungu vya Bajeti katika mfumo wa BAMAS. Vile vile, uratibu wa mradi wa ukarabati wa nyumba ya Wazee Limbani ulifanyika. Sambamba na hilo Wizara ilizitembelea na kuzitambua jumuiya 16 zisizo za

kiserikali (NGOs na CSOs) ili kubainisha maeneo ya ushirikiano, mafanikio na changamoto.

45. **Mheshimiwa Spika,** ripoti saba zimeandaliwa zikiwemo nne za utekelezaji wa kazi za Wizara na tatu zilizohusu utekelezaji wa Bajeti kwa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango. Aidha, ushirikiano wa kiutendaji baina ya Ofisi Kuu Pemba na Ofisi za Mkoa wa Kaskazini na Kusini Pemba umeendelea kutekelezwa.

**Programu ya Maendeleo ya Jamii na Jinsia (PH0403)**

46. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii inasimamia masuala ya Maendeleo ya Jamii, kukuza usawa wa Kijinsia na utekelezaji wa haki za Wanawake, Wanaume na Watoto. Programu hii ilitengewa shilingi 5,737,003,000.00. Hadi kufikia Machi, 2026 shilingi 7,520,949,688.00 zilipatikana ikiwa ni sawa na asilimia 131 ya makadirio. Aidha, Programu hii inasimamia utekelezaji wa Sera na Sheria zinazohusu Maendeleo ya Jamii kwa kuzingatia Mipango ya Kitaifa, Mikataba ya Kikanda na Kimataifa. Shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kama zifuatazo: -

i. Kuyafikia Majukwaa yote ya uwezeshaji wanawake kiuchumi kuanzia ngazi ya Shehia hadi Mikoa;

ii. Kuwajengea uwezo wanawake kuweza kuchukua fursa mbalimbali zikiwemo za kiuchumi, kisiasa na kijamii;

iii. Kuhamasisha Wanawake kushiriki kugombea nafasi za uongozi katika ngazi mbalimbali;

iv. Kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Kitaifa wa Kumaliza Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji dhidi ya

Wanawake na Watoto (NPA VAWC II), GEF, Mpango wa HeForShe na Mradi wa Mapambano dhidi ya Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Wasichana; na

v. Kuadhimisha siku za kimataifa na kikanda.

47. **Mheshimiwa Spika,** Wizara iliendelea kutekeleza programu mbalimbali za kuwawezesha wanawake na jamii kwa ujumla kupitia mafunzo, mikopo na huduma za kijamii. Vikundi 75 vya ushirika vilipatiwa elimu ya upatikanaji wa mikopo, huku wanawake wajasiriamali 195 wakipata mafunzo ya ujasiriamali na usimamizi wa mikopo ili kuongeza kipato na kupunguza utegemezi.

48. **Mheshimiwa Spika,** Wizara pia iliandaa ripoti ya Kimataifa ya CSW 70 na kutoa elimu ya msaada wa kisaikolojia na kijamii kwa wanawake katika wilaya mbalimbali za Unguja na Pemba. Waratibu wa wanawake na watoto pamoja na viongozi wa majukwaa walipewa mafunzo kuhusu usimamizi na uandishi wa taarifa, sambamba na mafunzo ya biashara mtandaoni, masoko na mikopo.

49. **Mheshimiwa Spika,** Kupitia Programu ya Dkt. Mwinyi Boosting Fund, wanawake wajasiriamali 4,026 wamenufaika na mikopo hiyo ambapo jumla ya shilingi 2,008,100,000.00 zimetolewa kwa wajasiriamali hao. Aidha, wanawake na vijana 23 walipata mafunzo ya ufundi stadi na vitendea kazi vyenye thamani ya shilingi milioni 23.

50. **Mheshimiwa Spika,** katika kupambana na ukatili wa kijinsia, kampeni za msaada wa kisheria, kisaikolojia, kijamii na kiuchumi zilifanyika Zanzibar nzima, ambapo malalamiko 254

yalipokelewa na wahanga kupatiwa huduma. Wananchi 8,633 walielimishwa kuhusu madhara ya ukatili wa kijinsia na haki za wanawake na watoto kupitia mikutano mbalimbali.

51. **Mheshimiwa Spika,** Vilevile, vijana wenye ulemavu, waandishi wa habari, maafisa wa mikoa na wilaya pamoja na wanafunzi wa Vyuo Vikuu walipatiwa mafunzo kuhusu ushiriki wa kijamii, kuripoti masuala ya GBV, matumizi salama ya intaneti na utekelezaji wa mipango ya kupambana na ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

52. **Mheshimiwa Spika,** Huduma ya Simu kwa Mtoto iliendelea kutoa msaada kwa watoto kupitia ushauri nasaha na kushughulikia kesi mbalimbali za ukatili, ubakaji, ndoa za utotoni na utelekezaji. Aidha, Programu ya HeForShe iliwafikia washiriki 400 kwa lengo la kuhamasisha usawa wa kijinsia, huku Wizara ikiendelea kuratibu Programu ya Kizazi Chenye Usawa (GEF) na shughuli nyingine za maendeleo ya jamii kwa kushirikiana na taasisi za Serikali na washirika wa maendeleo.

## D. MWELEKEO WA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2026/2027

### a. Malengo ya Wizara

53. **Mheshimiwa Spika,** mwelekeo wa utekelezaji wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa mwaka wa fedha 2026/2027 umezingatia maelekezo yaliyotolewa na Serikali katika kuimarisha utoaji wa huduma. Wizara itahakikisha kwamba huduma zinaendelea kuimarishwa pamoja na kutia nguvu zaidi kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia na kustawisha jamii. Kwa muktadha huo, vipaumbele vya Wizara vinagusa maeneo yafuatayo: -

i. Kuimarisha utekelezaji wa Mipango na Mikakati mbalimbali ya Wizara ikiwemo Mpango wa Pili wa Kitaifa wa Kupambana na Ukatili na Udhalilishaji dhidi ya Wanawake na Watoto (NPA VAWC II 2025 - 2030); Mpango wa Pili wa Utekelezaji wa Sera ya Hifadhi ya Jamii; na mikakati ya kuwawezesha wanawake kiuchumi, kisiasa na kijamii ikiwemo kufanyia kazi mpango wa utekelezaji wa Ahadi za Nchi za Kizazi Chenye Usawa GEF).

ii. Kuendelea kufanyia kazi Majukwaa ya Kuwawezesha Wanawake Kiuchumi kwa kuyaunganisha na fursa mbalimbali;

iii. Kutayarisha na kutekeleza Mpango wa Utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Jamii, kukamilisha mapitio ya Sera ya Jinsia na kukamilisha Sheria mpya ya Watoto;

iv. Kuimarisha mifumo na huduma za malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto katika ngazi za familia, jamii na taasisi;

v. Kuimarisha Hifadhi ya Jamii, Wazee, Watoto na Familia zinazoishi katika mazingira magumu zaidi, pamoja na kusimamia Pencheni Jamii na Mabaraza ya Wazee;

vi. Kuhamasisha jamii na taasisi kutumia Mapendekezo ya Utafiti wa Ukatili na Udhalilishaji dhidi ya Watoto na Vijana (VACS 2024) katika kuandaa programu na mipango yao;

vii. Kuratibu utoaji wa huduma za msingi kwa watu wenye mahitaji maalum ikiwemo huduma za msaada wa kisaikolojia kwa manusura wa majanga mbalimbali na makundi mengine yenye uhitaji katika jamii;

viii. Kuimarisha uratibu na usimamizi wa Kada za Ustawi na Maendeleo ya Jamii likiwemo suala la kutayarisha Sheria ya Ustawi wa Jamii;

ix. Kuratibu Mipango na bajeti inayozingatia Usawa wa Kijinsia katika Wizara, Taasisi, Mikoa na Wilaya; na

x. Kuimarisha nguvu kazi na mazingira ya kazi ikiwemo upatikanaji wa vitendea kazi, ukarabati wa majengo na utunzaji wa kumbukumbu muhimu za kiutumishi.

**b. Makadirio ya Mapato ya Wizara**

**54.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imekadiriwa kukusanya shilingi **15,000,000.00** kuchangia mfuko Mkuu wa Serikali.

**c. Mwelekeo wa Matumizi kwa Programu**

**55.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara imekadiriwa kutumia shilingi 26,574,601,000.00. Kati ya fedha hizo shilingi 9,679,560,000.00 sawa na asilimia 36, ni za Matumizi ya Kawaida, (zinazohusisha Mishahara shilingi 4,490,600,000.00, shilingi 5,188,960,000.00 za matumizi mengineyo inayohusisha pia shilingi 20,000,000 za Ruzuku kutoka kwa Washirika wa Maendeleo); na shilingi 16,895,041,000.00, sawa na asilimia 64 za maendeleo (zinazohusisha shilingi 7,000,000,000.00 kutoka SMZ, shilingi 891,300,000.00 Ruzuku za Maendeleo kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na Shilingi 9,003,700,000.00 ni Mkopo kutoka Benki ya Dunia). Angalia Kiambatanisho nambari 2 kinahusika.

### d. Miradi na Programu za Maendeleo

**56.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa Fedha 2026/2027, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto itatekeleza miradi na programu kama ifuatavyo:-

i. Kuendelea na ukarabati wa majengo ya Makaazi ya Wazee Sebleni;

ii. Kuendelea kutekeleza Mapambano Dhidi ya Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto kupitia Mradi wa TOKOMEZA unaotekelezwa kwa ushirikiano na UN Women na Programu inayotekelezwa kupitia ushirikiano na UNFPA;

iii. Kusimamia utekelezaji wa Mradi wa Kukuza Usawa wa Kijinsia Tanzania (PAMOJA). Mradi huu unahusisha maeneo makuu manne ya kiutekelezaji ambapo shabaha zilizopangwa ni:-

(a) Kutoa Mafunzo ya kuviandaa Vikundi vya Wanawake 640 vitakavyojumuisha wastani wa Wanavikundi 6,400 ili kuwajengea uwezo wa kusimamia shughuli zao za ujasiriamali na kuwezesha vikundi 240 kupokea mikopo;

(b) Kujenga Nyumba Salama mbili zitakazojengwa Unguja na Pemba;

(c) Kujenga Vituo vinane vya Malezi na Makuzi ya Awali ya Watoto Unguja na Pemba; na

(d) Usimamizi na Uratibu wa Mradi.

**Programu ya Hifadhi ya Jamii (PH0401)**

**57. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara imepanga kutumia shilingi 8,621,231,000.00, sawa na asilimia 32 ya makadirio ya bajeti ya Wizara kwa kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuendelea kutoa huduma za kiustawi kwa Wazee ikiwemo kufanyia kazi upatikanaji na matumizi ya vitambulisho na kuimarisha mabaraza ya wazee katika maeneo yao ya makaazi;

ii. Kuendelea na awamu ya pili ya matengenezo katika makaazi ya wazee Sebleni na kujenga makaazi ya wazee ya Welezo;

iii. Kutoa huduma za hifadhi na ustawi wa jamii kwa watu wenye mazingira magumu zaidi; na

iv. Kutekeleza Mpango wa Malezi na Makuzi ya Awali ya Watoto (ECD).

**Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara (PH0102)**

**58. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara imepanga kutumia shilingi 7,037,890,000.00, sawa na asilimia 26.5 ya makadirio ya bajeti ya Wizara.

***Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji (SH040201)***

**59. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kuendelea kuwajengea uwezo watumishi wa Wizara na kuwapatia haki na stahiki zao;

ii. Kuendelea kuimarisha usimamizi wa shughuli za utawala na uendeshaji wa Ofisi ikiwa ni pamoja na kuipatia Wizara vitendea kazi;

iii. Kuendelea kuimarisha kumbukumbu na nyenzo nyingine za kiutumishi kwa kutumia Mifumo ya TEHAMA iliyopo ili kuweka usimamizi imara wa rasilimali watu katika Wizara; na

iv. Kuendelea kuimarisha na kusimamia dhana ya Uwajibikaji unaozingatia misingi ya Kiutumishi na Utawala bora.

***Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti (SH040202)***

**60. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Programu Ndogo hii imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kuratibu utayarishaji wa Mipango, Bajeti na Ripoti za Wizara;

ii. Kuandaa na kuchambua sera zinazosimamiwa na Wizara na Sera nyingine za Kisekta ili kuhakikisha dhana ya maendeleo ya jamii, mipango na bajeti inayozingatia jinsia zinaendelea kukondoishwa. Idara itaendelea kuratibu utayarishaji wa Programu ya Usawa wa Kijinsia na Maendeleo kwa ushirikiano na Taasisi ya Bufdir ya Norway;

iii. Kushiriki na kuandaa vikao na Wadau – Washirika wa Maendeleo, NGO's, Taasisi za Kiserikali na Zisizo za Kiserikali),

iv. Kuendelea kuratibu ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Wizara na kutekeleza mikakati ya kufanyia kazi tafiti za kijamii.

### *Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji Ofisi Kuu Pemba (SH040203)*

61. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara imepanga kutekeleza yafuatayo: -

    i. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli za kawaida za Wizara Pemba ikiwemo shughuli zinazohusu Ustawi na Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto;

    ii. Kuratibu na kusimamia utekelezaji wa sera, sheria, miongozo na kanuni za Wizara; na

    iii. Kuwajengea uwezo watumishi, kuweka mazingira mazuri ya kazi pamoja na kuhakikisha haki na stahiki zao.

### Programu ya Maendeleo ya Jamii na Jinsia (PH0403)

62. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara imepanga kutumia shilingi 10,915,480,000.00, sawa na asilimia 41 ya makadirio ya bajeti ya Wizara. Programu ya Maendeleo ya Jamii na Jinsia imepanga kutekeleza yafuatayo: -

    i. Kuratibu na kusimamia Utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Jamii;

    ii. Kukuza ukondoishaji (Gender Mainstreaming) wa masuala ya Jinsia sambamba na uwezeshaji wa wanawake kiuchumi kupitia majukwaa ya uwezeshaji wanawake Kiuchumi.

    iii. Kupambana na vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji wa wanawake na watoto kwa kuendelea kutekeleza Mpangokazi wa Kitaifa wa Kupambana na Ukatili na Udhalilishaji Dhidi ya Wanawake na Watoto (NPA – VAWC II).

iv. Kujenga uelewa kwa wanaume juu ya masuala ya kuwasaidia wanawake ili kukuza usawa wa Kijinsia kwa kuhuisha Program ya Kizazi Chenye Usawa – GEF na HeForShe – Wanaume wa Mabadiliko ndani ya Jamii na Taasisi zinazotoa huduma.

v. Kusimamia utawala bora na uwajibikaji kwa mabaraza ya watoto ngazi zote (Shehia, Wilaya na Taifa) sambamba na kuwajenga watoto katika misingi ya uzalendo, kujitambua, kutambua falsafa za uongozi, haki na wajibu wao kwa ujumla.

## E. SHUKURANI

63. **Mheshimiwa Spika,** nachukua fursa hii kutoa shukrani kwa taasisi mbalimbali za Serikali, mashirika yasiyo ya Serikali, washirika wa maendeleo, sekta na watu binafsi kwa mchango wao katika kufanikisha shughuli za maendeleo na ustawi wa jamii, wanawake, watoto, vijana na wazee kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

64. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa shukrani za pekee kwa chama changu, Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa ngazi zake zote na Jumuiya zake (UWT, UVCCM na WAZAZI) kwa kusimamia vyema utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 – 2025. Ninaishukuru kwa dhati jumuiya ya wanawake Tanzania (UWT) na Kamati ya Kitaifa ya Mapambano ya Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia ya UWT. Aidha, ninazishukuru Wizara na Taasisi zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mashirikiano yao waliyoipatia Wizara yangu katika mwaka wa fedha 2025/2026. Ninaishukuru Taasisi ya Ofisi ya Rais inayosimamia Utekelezaji Serikalini

(PDB) na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali; Wizara ya Afya; Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo; na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum katika ushirikiano wa kuimarisha malezi na makuzi ya awali ya mtoto. Naishukuru Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mashirikiano wanayotupatia pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais na Wizara zote za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

65. **Mheshimiwa Spika,** Wizara inatambua mchango wa mashirika ya kimataifa na washirika wa maendeleo wakiwemo Italy, Norway, Finland, Umoja wa Falme za Kiarabu - UAE, Umoja wa Ulaya - EU, World Bank, UNICEF, UNFPA, WHO, USAID, Qatar Foundation, UN-WOMEN, UNESCO, HelpAge Tanzania, Noah Foundation/Good People, SOS, IOM, Save the Children; Afisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, ZEEA, ZBS, SUZA, ZU, Chuo Kikuu cha SUMAIT, Maisha Bora Foundation, Mwanamke Initiative, JUWAZA, JUYAWAZA, JUWAUZA, C-Sema, ZASWA, CRF, ZAMWASO, ZASO, ZACA, ZAPHA+, BAKIZA, Kampuni ya Simu YAS, na wote ambao tunaendelea kushirikiana nao; pamoja na taasisi za kifedha, elimu, sheria na maendeleo ya jamii zilizoshiriki katika kusaidia utekelezaji wa programu za Wizara.

66. **Mheshimiwa Spika,** natoa shukrani kwa Viongozi na Watumishi wote wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa ushirikiano na juhudi zao katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Aidha, natoa shukrani kwa familia yangu kwa msaada na uvumilivu walionipa katika kutekeleza wajibu wangu wa kiuongozi.

## F. HITIMISHO

**67.** **Mheshimiwa Spika,** natoa shukurani za dhati kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa **Dkt. Hussein Ali Mwinyi** kwa kuendelea kuiongoza vyema nchi yetu na kutuletea maendeleo makubwa. Vile vile, nakushukuru Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Naibu Spika kwa uongozi wenu wa Baraza letu la Wawakilishi.

**68.** **Mheshimiwa Spika,** naomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu waichangie hotuba hii, watushauri ipasavyo na hatimaye waiidhinishie Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto matumizi ya shilingi 26,574,601,000.00 ili kutekeleza kazi za kawaida na kazi za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Aidha, Mheshimiwa Spika, naliomba Baraza lako tukufu liikubalie Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ichangie kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali shilingi 15,000,000.00.

**69.** **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

……………………

**ANNA ATHANAS PAUL (MBM)**
**WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO ZANZIBAR**

## Kiambatanisho Nam. 1: Muhtasari wa Upatikanaji wa Fedha kwa Kipindi cha Julai, 2025 - Machi 2026

| | Fedha Zilizopangwa (000) | | | | Fedha zilizopatikana (000) | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Prongramu** | **Jumla** | **Mishahara** | **Matumizi Mengineyo** | **Miradi** | **Jumla** | **Mishahara** | **Matumizi Mengineo** | **Miradi** | **%** |
| Programu Utawala na Uendeshaji | **7,691,815** | 4,196,100 | 3,495,715 | | **4,094,716** | 3,156,786 | 937,930 | | **53%** |
| ProgramNdogo Utawala na Uendeshaji | **5,553,920** | 3,590,405 | 1,963,515 | | **3,212,667** | 2,692,106 | 520,562 | | **58%** |
| Programu ndogo Mipango, Sera na Utafiti | **432,100** | | 432,100 | | **37,777** | | 37,777 | | **9%** |
| Afisi Kuu Pemba | **1,705,795** | 605,695 | 1,100,100 | | **844,271** | 464,680 | 379,591 | | **49%** |
| Programu ya Hifadhi Ya Jamii | **3,643,223** | | 1,980,934 | 1,500,000 | **2,160,425** | | 956,096 | 1,204,329 | **59%** |
| Programu ya Maendeleo ya Jamii na Jinsia | **5,737,003** | | 746,482 | 4,990,521 | **7,520,949** | | 782,518 | 6,738,432 | **131%** |
| **Jumla Kuu** | **17,072,042** | **4,196,100** | **6,397,639** | **6,490,520** | **13,776,091** | **3,156,786** | **2,676,545** | **7,942,760** | **81%** |

Chanzo: WMJJWW, 2025/2026

## Kiambatanisho Nam. 2: Mwelekeo wa Bajeti kwa mwaka 2026/2027

| FUNGU /IDARA | KAZI ZA KAWAIDA ('000) | | | KAZI ZA MAENDELEO ('000) | | | | JUMLA KUU |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | JUMLA KUU | MISHAHARA NA STAHIKI | MATUMIZI MENGINEYO | SMZ | WAHISANI | | JUMLA MAENDELEO | |
| | | | | | UN WOMEN | WB | | |
| **PH0401 Hifadhi ya Jamii** | **1,621,231** | | **1,621,231** | **7,000,000** | | | **7,000,000** | **8,621,231** |
| | | | | | | | | |
| **PH0402 utawala na Uendeshaji** | **7,037,890** | **4,490,600** | **2,547,290** | | | | | **7,037,890** |
| SH040201 Utawala na Uendeshaji | 5,157,670 | 3,817,010 | 1,340,660 | | | | | 5,157,670 |
| | | | | | | | | |
| SH04202 Mipango Sera Na Utafiti | 402,210 | | 402,210 | | | | | 402,210 |
| | | | | | | | | |
| SH040203 Utawala na Uendeshaji Afisi Kuu Pemba | 1,478,010 | 673,590 | 804,420 | | | | | 1,478,010 |
| | | | | | | | | |
| **PH0403 Maendeleo ya Jamii na Jinsia** | **1,020,439** | | **1,020,439** | | **636,321** | **9,258,720** | **9,895,041** | **10,915,480** |
| **JUMLA** | **9,679,560** | **4,490,600** | **5,188,960** | **7,000,000** | **636,321** | **9,258,720** | **16,895,041** | **26,574,601** |
| **JUMLA KUU** | **26,574,601** | **4,990,600** | **5,188,960** | **7,000,000** | **636,321** | **9,258,720** | **16,895,041** | **26,574,601** |

Chanzo: WMJJWW, 2025/2026

**Kiambatanisho Nam. 3: Taarifa ya Wazee walio katika Mpango wa Pencheni Jamii**

| Wilaya | KE | ME | Jumla | Wapya | Waliofariki |
|---|---|---|---|---|---|
| Kaskazini "A" | 2,290 | 1,569 | 3,859 | 261 | 110 |
| Kaskazini "B" | 1,095 | 766 | 1,861 | 114 | 64 |
| Kati | 1,125 | 981 | 2,106 | 133 | 88 |
| Kusini | 779 | 510 | 1,289 | 62 | 20 |
| Magharibi "A" | 1,256 | 945 | 2,201 | 189 | 44 |
| Magharibi "B" | 1,536 | 1,286 | 2,822 | 211 | 73 |
| Mjini | 3,122 | 2,661 | 5,783 | 423 | 235 |
| **Jumla Unguja** | **11,203** | **8,718** | **19,921** | **1,393** | **634** |
| Chake chake | 1,927 | 1,416 | 3,343 | 178 | 171 |
| Micheweni | 1,761 | 1,246 | 3,007 | 307 | 83 |
| Mkoani | 1,960 | 1,377 | 3,337 | 245 | 83 |
| Wete | 2,542 | 1,731 | 4,273 | 355 | 134 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Jumla Pemba | 8,190 | 5,770 | 13,960 | 1,085 | 401 |
| Jumla Kuu | 19,393 | 14,488 | 33,881 | 2,478 | 1,035 |

Chanzo: WMJJWW, 2025/2026

## Kiambatanisho Nam. 4: Malalamiko ya Matunzo na Mvutano wa Malezi

| **Aina ya Malalamiko/Zanzibar** | **Yaliyoripotiwa** | | **Yaliyopatiwa ufumbuzi** | | **Yaliyopelekwa Rufaa** | | **Yanayoendelea na Usuluhishi** | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Ung | Pba | Ung | Pba | Ung | Pba | Ung | Pba |
| Matunzo | 238 | 152 | 133 | 77 | 60 | 3 | 45 | 71 |
| Mvutano wa Malezi | 168 | 99 | 88 | 68 | 53 | 5 | 27 | 26 |
| **Jumla** | **406** | **251** | **221** | **145** | **113** | **8** | **72** | **97** |

Chanzo: WMJJWW, 2025/26

## Kiambatanisho Nam. 5: Wahanga waliopo Nyumba Salama

| **Sababu za Kupokewa Kwenye Nyumba** | **Jinsia** | | **Umri** | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|
| | **Ke** | **Me** | | |
| Usafirishaji Haramu | 17 | | 08-17 | 17 |
| Kutoroka | 3 | 4 | 10-18 | 7 |
| Kukosa Matunzo | 2 | 4 | 1-17 | 6 |
| Kupigwa | 2 | 1 | 3-25 | 3 |
| Kuingiliwa kinyume ya maumbile | 1 | 0 | 13 | 1 |
| Mvutano wa malezi | 1 | 0 | 32 | 1 |
| Kubakwa | 2 | 0 | 10-12 | 2 |
| Kakataa Ndoa | 1 | 0 | 18 | 1 |
| Kufika Unguja kutafuta kazi | 1 | 1 | 11-27 | 2 |
| Kazi za majumbani | 5 | 0 | 13-16 | 5 |
| Omba omba | 3 | 1 | Miezi 7-26 | 4 |
| **Jumla** | **38** | **11** | | **49** |

Chanzo: WMJJWW, 2025/2026

## Kiambatanisho Nam. 6: Vituo Vya Kulelea Watoto Yatima

| Jina la Kituo | Ke | Me | Idadi ya Watoto | Eneo la Kituo |
|---|---|---|---|---|
| Mazizini | 9 | 20 | 29 | Mazizini |
| Fatima House | 18 | 22 | 40 | Jumbi |
| Kiidundo Orphanage Centre | 12 | 15 | 27 | Tunguu |
| Island Hope Foundation | 6 | 10 | 16 | Chukwani |
| Daru- Al- Ahbaab | 0 | 41 | 41 | Micheweni/ Pemba |
| Sakina Girls Home | 0 | 20 | 20 | Jumbi |
| Salim Turkey Foundation | 68 | 0 | 68 | Kandwi |
| Assalam Orphanage Foundation | 10 | 16 | 26 | Meli tano |
| ZASO Children's Home | 27 | 20 | 47 | Fuoni mambosasa |
| Al- maftuh Foundation "A" | 25 | 22 | 47 | Kibele |
| Amani Foundation | 20 | 10 | 30 | Chukwani |
| Al- nassir Foundation | 18 | 0 | 18 | Jumbi |
| Markazyl Yaqeen | 0 | 35 | 35 | Kinduni |
| Rahmatu Al- Khair Orphanage Centre | 0 | 89 | 89 | Kibele |
| Maftuh Foundation"B" | 18 | 12 | 30 | Kidimni/kitumba |
| Montesori Orphanage Centre | 15 | 12 | 27 | Bububu |
| PDS Children's Home | 9 | 0 | 9 | Jendele |
| Muzammil Orphanage Centre | 10 | 15 | 25 | F/ Meli tano |
| Jumla | **265** | **359** | **624** | |

Chanzo WMJJWW 2025/2026

**Kiambatanisho Nam. 7: Orodha ya walezi wa malezi na watoto waliopo katika malezi**

| Wilaya | Idadi ya Walezi | Idadi ya watoto | | Jumla | Walioingia | Waliotoka |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ke | Me | | | |
| Mjini | 29 | 13 | 6 | 19 | 0 | 0 |
| Magharibi "A" | 20 | 8 | 5 | 13 | 2 | 0 |
| Magharibi "B" | 26 | 7 | 14 | 21 | 0 | 1 |
| Kaskazini "A" | 12 | 1 | 1 | 2 | 0 | 0 |
| Kaskazini"B" | 24 | 5 | 1 | 6 | 0 | 3 |
| Mkoani | 25 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Chakechake | 15 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 |
| Micheweni | 29 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 |
| Wete | 26 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **206** | **34** | **29** | **63** | **02** | **4** |

Chanzo WMJJWW 2025/2026

**Kiambatanisho Nam. 8a: Idadi ya Watumishi wa Wizara**

| Eneo | Ke | Me | Jumla |
|---|---|---|---|
| **Unguja** | **171** | **100** | **271** |
| **Pemba** | **25** | **20** | **45** |
| **Jumla** | **196** | **120** | **316** |

Chanzo: WMJJWW 2025/2026

**Kiambatanisho Nam. 8b: Watumishi waliopo kwenye mafunzo ya muda mrefu**

| Aina ya Masomo | Jinsi | | Jumla |
|---|---|---|---|
| | Ke | Me | |
| Utawala | 1 | 0 | 1 |
| Sayansi na IT | 0 | 2 | 2 |
| Sheria | 1 | 0 | 1 |
| Ushauri Nasaha | 0 | 1 | 1 |
| Afya ya Jamii | 1 | 0 | 1 |
| Waendesha Ofisi | 1 | 0 | 1 |
| **JUMLA** | **4** | **3** | **7** |

Chanzo WMJJWW, 2025/2026

**Kiambatanisho Nam. 8c: Watumishi waliopatiwa mafunzo ya muda mfupi**

| Aina ya Masomo | Idadi ya Watumishi | | |
|---|---|---|---|
| | Ke | Me | Jumla |
| Kumbukumbu na nyaraka | 1 | 1 | 2 |
| Mfumo wa PSMIS | 1 | 0 | 1 |
| *Impact 0f 2030 agenda for Sustainable development for developing Country Women and Children* | 0 | 2 | 2 |
| Matumizi ya Kiswahili Fasaha kwa waendeshaji Ofisi | 4 | 0 | 4 |
| *Strategic Succession plan and Human Resource Auditing* | 0 | 1 | 1 |
| Udereva | 0 | 1 | 1 |
| **Jumla** | **6** | **5** | **11** |

Chanzo WMJJWW, 2025/2026